JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

MPANGO KAZI WA UFUATILIAJI NA TATHMINI KWA MWAKA 2023/24

JULAI, 2023

YALIYOMO

MUHTASARI ..... *iv*

SEHEMU YA KWANZA *1*

UTANGULIZI *1*

1.1 Chimbuko **1**

1.2 Umuhimu wa Mpango kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini **1**

1.3 Majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo **2**

1.4 Idara na Vitengo vya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ... **2**

1.5 Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo 3

1.6 Lengo la Mpangokazi wa Ufuatiliaji na Tathmini **3**

1.6.1 Lengo Kuu **3**

1.6.2 Malengo Mahsusi **3**

1.7 Matokeo ya Utekelezaji wa Mpangokazi wa Ufuatiliaji na Tathmini 3

SEHEMU YA PILI *5*

MAENEO MAHSUSI NA RATIBA YA UFUATILIAJI NA TATHMINI *5*

KWA MWAKA 2023/24 ..... *5*

2.1 Utangulizi **5**

SEHEMU YA TATU **11**

MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIWA KATIKA UFUATILIAJI NA TATHMINI ***11***

3.1 Utangulizi **11**

3.2 Majukumu ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini **11**

3.3 Kujenga uwezo wa Watumishi Wizara katika masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini **11**

3.4 Utaratibu wa Idara/ Vitengo na Wadau Wengine Kushiriki katika Ufuatiliaji na Tathmini **11**

3.5 Mtiririko wa Hatua za Utekelezaji wa Shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini **12**

3.6 Zana kwa Ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini **12**

3.7 Muundo wa Taarifa ya Ufuatiliaji na Tathmini **12**

3.8 Ufuatiliaji wa Viashiria **13**

3.9 Ufuatiliaji na tathmini ya Vihatarishi **13**

3.10 Tathmini **13**

3.11 Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini **13**

3.12 Utaratibu wa Upatikaji wa Fedha za Utekelezaji wa Mpango wa Ufatiliaji na Tathmini kwa Mwaka 2023/24 ..... **14**

SEHEMU YA NNE ***15***

HITIMISHO*.....*15

MUHTASARI

Mpangokazi wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo umeainisha shughuli, muda/na wadau wa ufuatiliaji na tathmini wa miradi ya maendeleo pamoja na kazi nyingine muhimu zinazotelezwa na kuratibiwa na Wizara katika mwaka 2023/24.

Maandalizi ya Mpango U&T yanalenga kuimarisha mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini ndani ya Wizara. Aidha, ni zingatio la Sheria na Miongozo mbalimbali inayosimamia utumishi wa Umma ikijumuisha Sheria ya Bajeti Sura 439; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2023/24; Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini katika Utumishi wa Umma; Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo; na Mkakati wa ufuatiliaji wa Tathmini za Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano - FYDP III (2021/22-2025/26). Sanjari na miongozo hiyo, pia suala la ufuatiliaji na tathmini limesisitizwa na Serikali Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hasa baada ya kufanyika mabadiriko ya muundo wa Idara za Sera na Mipango kwa kupandisha hadhi Sehemu ya Ufuatiliaji na Tathmini zilizokuwa ndani ya Idara za Sera na Mipango vikiongozwa na Wakurugenzi Wasaidizi na kuwa Vitengo Kamili vinavyoongozwa na Mkurugenzi ili kuviwezesha vitengo hivi kuwa na uwezo kamili wa kufuatilia utekelezaji wa majukuku, miradi na Programu mbalimbali zinazotekelezwa na Wizara katika kipindi husika. Hivyo, katika kipindi cha mwaka 2023/24, majukumu ya Ufuatiliaji na Tathmini yataratibiwa na Kitengo kipya cha Ufuatiliaji na Tathmini kuanzia mwezi Julai, 2023

Uwepo kwa Mpangokazi huu utawezesha ufanisi na tija katika jukumu la uratibu wa shughuli za Wizara *(informed decision making)* na hatimaye kufanikisha azma ya Wizara kutoa huduma stahiki kwa Wadau. Hatua hii italeta tija katika utoaji huduma kwa wadau wa sekta, kuzalisha ajira, fedha za kigeni, kodi, kupunguza gharama za matibabu hususan magonjwa yasioambukiza, utalii, mazingira, kulinda utambulisho wa utamaduni wa jamii, historia ya Tanzania, kukuza mahusiano ya Kikanda na Kimataifa, na kukuza diplomasia uchumi baina ya nchi kupitia michezo.

Mwisho, naelekeza Idara na Vitengo vya Wizara kutekeleza kikamilifu Mpango kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini ili kufanikisha malengo ya Wizara.

Saidi Yakubu, **FCG**
KATIBU MKUU

SEHEMU YA KWANZA

UTANGULIZI

1.1 Chimbuko

Mpangokazi wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo umeainisha shughuli, muda/na wadau wa ufatiliaji na tathmini wa miradi ya maendeleo pamoja na kazi nyingine muhimu zinazotekelezwa na kuratibiwa na Wizara katika mwaka 2023/24. Mpango huu unalenga kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa majukumu ya Wizara ili kupima utendaji kwa kuzingatia bajeti iliyotengwa kwa kila Kasma na hatimaye kupata thamani ya pesa itakayotumika.

Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na Programu za Maendeleo, unaelekeza Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma kuandaa na kuzingatia Mpango Kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini. Aidha, hili ni sehemu ya utekelezaji wa Sheria ya Bajeti, Sura 439 na Kanuni zake.

Aidha, endapo Mpango Kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini utatekelezwa ipasavyo utakuwa muafaka katika kusaidia kubainisha thamani ya pesa iliyotumika *(value for money)* na kuhuisha mipango ya utekelezaji kurejewa kwa sera za sekta .

1.2 Umuhimu wa Mpango kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini

Kuwepo kwa Mpangokazi huu utawezesha ufanisi na tija katika jukumu la uratibu wa shughuli za Wizara zikiwemo Taasisi zilizo chini yake na hatimaye kufanikisha azma ya Wizara kutoa huduma stahiki kwa Wadau. Hatua hii italeta tija katika kuzalisha ajira, fedha za kigeni, kodi, kupunguza gharama za afya (matibabu hususan magonjwa yasiyoambukiza), utalii, mazingira, kulinda utambulisho wa utamaduni wa jamii, historia ya Tanzania, kukuza mahusiano ya Kikanda na Kimataifa; na kukuza diplomasia uchumi baina ya nchi kupitia michezo

Msisitizo wa masuala ya ufuatiliaji na tathmini katika Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo umeanzia katika Muundo wa Wizara ambao unajumuisha Sehemu ya Ufuatiliaji na Tathmini itakayokuwa chini ya Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini. Aidha, Mpango Mkakati wa Wizara wa Mwaka 2021/22 - 2025/26 umetoa mwongozo wa ufuatiliaji na tathmini ambapo unawezesha kupima matokeo *‘Outcome results’* yatakayotokana na utekelezaji wa shughuli za Wizara kwa kipindi cha miaka mitano (5).

Pamoja na kuwa kila mwaka Wizara imeendelea kutekeleza masuala ya ufuatiliaji na tathmini kwa mujibu wa miongozo mbalimbali ya Kitaifa, Wizara imeandaa huu ili kuondoa changamoto zilizojitokeza ikiwemo: **Idara na Vitengo vya Wizara, kutoandaa taarifa baada ya kufanya ufuatiliaji na tathmini; kutofanyika kwa**

tathmini kwa masuala ya kimkakati na muhimu yanayosimamiwa na Wizara; kuwepo kwa urudufu wa Idara na Vitengo katika ufanyaji wa shughuli za Ufuatiliaji; Idara na Vitengo kutojua wajibu wao na masuala ya kuzingatia katika kufanya ufuatiliaji na tathmini; gharama kubwa za ufuatiliaji kutokana na kutokuwa na uratibu wa pamoja wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini baina ya Idara na Vitengo; na kukosekana kwa taarifa na takwimu muhimu za utekelezaji wa baadhi wa masuala muhimu wakati wa kufanya maamuzi kutokana na kutokufanyiwa ufuatiliaji na tathmini.

Hivyo, Mpango kazi wa ufuatiliaji wa tathmini utatatua changamoto zilizopo na kuimarisha utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini kwa Idara na Vitengo vya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo.

1.3 Majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Mpangokazi huu utawezesha utekelezaji wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini na kupima matokeo ya utekelezaji wa majukumu ya Wizara ambayo ni:-

(a) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Mipango mbalimbali ya Serikali katika Sekta za Utamaduni, Sanaa na Michezo;
(b) Kuendeleza Sekta za Sanaa, Filamu, Utamaduni na Michezo nchini;
(c) Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara.
(d) Kusimamia utendaji kazi wa Asasi, Miradi na Programu zilizo chini ya Wizara ;
(e) Kuratibu na kusimamia maendeleo ya utamaduni, sanaa na michezo nchini; na
(f) Kuendeleza, kuwezesha na kuratibu masuala ya kuwajengea uwezo watumishi ili watekeleze majukumu yao kikamilifu

1.4 Idara na Vitengo vya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Shughuli zote za ufuatiliaji na tathmini na Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini. Hata hivyo, Idara na Vitengo vyote vya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo vinatekeleza jukumu la ufuatiliaji na tathmini katika maeneo yao na kuwasilisha taarifa za ufutiliaji na tathmini kwa Idara ya Sera na Mipango. Idara na Vitengo vya Wizara ni kama ifuatavyo:-

Idara

a) Idara ya Maendeleo Utamaduni;
b) Idara ya Maendeleo ya Sanaa;
c) Idara ya Maendeleo ya Michezo;
d) Idara ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu; na
e) Idara ya Sera na Mipango;

Vitengo

a) Kitengo cha Fedha na Uhasibu;
b) Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani;
c) Kitengo cha Mawasiliano Serikalini;
d) Kitengo cha Ugavi na Ununuzi;
e) Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano; na
f) Kitengo cha Huduma za Sheria.
g) Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini

1.5 Taasisi Zilizo Chini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo inatekeleza majukumu ya kisera kupitia Taasisi zilizo chini ya Wizara. Hivyo, shughuli za ufuatiliaji na tathmini za Wizara zitahusisha miradi na shughuli za kimkakati zinazotekelezwa na Taasisi Saba (7) zilizo chini Wizara ambazo ni: -

(a) Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA)
(b) Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA)
(c) Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo (TaSUBa)
(d) Bodi ya Filamu na Michezo ya Kuigiza (TFB)
(e) Baraza la Michezo la Taifa (BMT)
(f) Ofisi ya Hakimiliki Tanzania (COSOTA); na
(g) Chuo cha Maendelo ya Michezo Malya.

1.6 Lengo la Mpangokazi wa Ufuatiliaji na Tathmini

1.6.1 Lengo Kuu

Lengo kuu la Mpango kazi ni kuweka mfumo wa pamoja wa uratibu wa ufuatiliaji na tathmini ya miradi na shughuli za Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo ili kupata tija na ufanisi katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka 2023/24.

1.6.2 Malengo Mahsusi

(a) Kuwepo uratibu wa pamoja (coordinated process) wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini kwa kazi zinazotekelezwa na Wizara kupitia Idara, Vitengo na Taasisi zilizochini ya Wizara;
(b) Kuimarisha ushiriki wa Idara na Vitengo katika shughuli za ufuatiliaji na tathmini;
(c) Kufanikisha Idara na Vitengo kutekeleza wajibu wao katika shughuli za ufuatiliaji na tathmini; na
(d) Kuwajengea uwezo wa Watumishi wa Wizara katika kufanya ufuatiliaji na tathmini.

1.7 Matokeo ya Utekelezaji wa Mpangokazi wa Ufuatiliaji na Tathmini

(a) Kuandaliwa kwa Mpango Kazi wa Ufuatiliaji na Tathmini ikiwa ni pamoja na maeneo msingi yatakayozingatiwa;
(b) Kuimarika kwa uwezo wa watumishi wa Idara ya Sera na Mipango na wengineo katika Wizara ikiwemo uelewa wa namna ya ufanyaji wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini;
(c) Kuimarika kwa utoaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini;
(d) Kufanyika kwa tathmini ya shughuli muhimu zinazosimamiwa na Wizara;
(e) Kuwezesha miradi na shughuli zinazosimamiwa na Wizara kwa ufanisi na kufikiwa kwa malengo yaliyokusudiwa;

(f) kuwezesha Wizara kufanya maamuzi sahihi na kwa wakati kulingana na masuala mbalimbali ya kimkakati yaliyoibuliwa ; na

(g) Kuimarika kwa utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa ajili ya uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 pamoja na maelekezo mbalimbali ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

SEHEMU YA PILI

MAENEO MAHSUSI NA RATIBA YA UFUATILIAJI NA TATHMINI KWA MWAKA 2023/24

2.1 Utangulizi

Sehemu hii inabainisha kazi zinazotekelezwa na *Kitengo cha* Ufuatiliaji na Tathmini kwa mwaka 2023/24. Kazi hizi zinajumuisha kazi za Wizara zilizoainishwa kupitia Mpango Kazi na Mpango wa Mtiririko wa Fedha wa Mwaka 2023/24; Mpango Mkakati wa Mwaka 2021/22 - 2025/26, Ilani ya CCM kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 - 2025/26); na Miradi inayoratibiwa na Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara. **Jedwali Na. 1 linaonesha maeneo mahsusi na ratiba ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Mwaka 2023/24.**

Jedwali Na. 1: Maeneo Mahsusi na na Ratiba ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa Mwaka 2023/24

Na.	Eneo Litakalofanyiwa Ufuatiliaji na Tathmini	Muda wa Utekelezaji na Tathmini				Mahali/Mkoa	Mhusika
		Robo ya I (Julai – Septemba, 2023)	**Robo ya II (Oktoba – Desemba, 2023)**	**Robo ya III Januari – Machi, 2024)**	**Robo ya IV (Aprili – Juni, 2024**		
1.	Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Mwaka 2023/24 kwa kuzingatia Mpango Kazi *(Action Plan)* na Mpango wa mtiririko wa Fedha *(cash flow plan)*	Septemba, 2023	Desemba, 2023	Machi, 2024	Juni, 2024	Dodoma	DME
2.	Kufuatilia utekelezaji wa majukumu ya Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika	Agosti, 2023	Desemba, 2023		Mei, 2024	DSM na Mikoa mingine	DME DPP MUT
3.	Kutembelea na kufuatilia Ofisi za Mfuko wa Utamaduni Tanzania pamoja na kukagua Maandalizi ya Ujenzi wa Jengo la Ofisi za Utamaduni na Sanaa.		Oktoba, 2023		Juni, 2024	DSM na Mikoa mingine	DME DPP MMS MUT
4.	Ujenzi wa Chuo cha Maendeleo ya Michezo Malya; na Ukarabati na Uendelezaji wa Academia ya Michezo		Novemba, 2023	Machi, 2024	Mei, 2024	Magu-Mwanza	DME DPP MMM
5.	Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma.		Novemba, 2023	Machi, 2024	Juni, 2024	Dodoma	DME DPP MMM

Na.	Eneo Litakalofanyiwa Ufuatiliaji na Tathmini	Muda wa Utekelezaji na Tathmini				Mahali/Mkoa	Mhusika
		Robo ya I (Julai – Septemba, 2023)	**Robo ya II (Oktoba – Desemba, 2023)**	**Robo ya III Januari – Machi, 2024)**	**Robo ya IV (Aprili – Juni, 2024**		
6.	Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi na Ujenzi wa *Sports Arena* (Dar es Salaam na Dodoma)		Novemba, 2023	Machi, 2024	Mei, 2024	Dar es Salaam na Dodoma	DME DPP MMM
7.	Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam.		Novemba, 2023	Machi, 2024	Mei, 2024	Dar es Salaam	DME DPP MMM
8.	Ujenzi na Uimarishaji wa Miundombinu ya Michezo katika Shule Maalum za Michezo		Desemba, 2023		Aprili, 2024	Mikoani	DME DPP MMM
9.	Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020-2025 kupitia Idara za Kisekta na Taasisi zilizochini yake kwa Kipindi kitakachobainishwa.	Agosti, 2023	Novemba, 2023	Machi, 2024	Juni, 2024	Dodoma	DME DPP MUT MMS MMM; na TAASISI
10.	Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo		Novemba, 2023	Machi, 2024	Juni, 2024	Bagamoyo-Pwani	DME DPP MMS
11.	Tathmini ya utekelezaji wa Mkataba wa Huduma kwa Mteja (CSC).				Machi, 2024	Dodoma	DAHRM
12.	Tathmini ya Bajeti ya Mishahara kwa kuangalia upandishwaji na, ubadilishwaji vyeo.			Februari, 2024		Dodoma	DAHRM

Na.	Eneo Litakalofanyiwa Ufuatiliaji na Tathmini	Muda wa Utekelezaji na Tathmini				Mahali/Mkoa	Mhusika
		Robo ya I (Julai – Septemba, 2023)	**Robo ya II (Oktoba – Desemba, 2023)**	**Robo ya III Januari – Machi, 2024)**	**Robo ya IV (Aprili – Juni, 2024**		
13.	Tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Uratibu wa Programu ya Kubidhaisha Kiswahili Duniani.		Desemba, 2023		Juni, 2024	Dar es Salaam	DME DPP MUT
14.	Tathmini matokeo ya matumizi ya vifaa vya ukalimani vilivyonunuliwa BAKITA.			Machi, 2024		Dar es Salaam	DME DPP MUT
15.	Tathmini ya Mifumo ya Usajili wa Kielekroniki (BASATA na Bodi ya Filamu Tanzania.		Desemba, 2023		Aprili, 2024	Dar es Salaam	DME DPP MUT MMS
16.	Tathmini ya Mifumo ya Kieletroki ya Ukusanyaji Mapato Uwanja wa Benjamin Mkapa na Uhuru.		Desemba, 2023			Dar es Salaam	DPP MMM
17.	Ufuatiliaji wa ujenzi wa Jengo la Wizara Awamu ya Pili -Mtumba	Septemba, 2023	Desemba, 2023	Aprili, 2024	Juni, 2024	Dodoma	DME DAHRM DPMU DPP
18.	Ufuatiliaji wa Utendaji kazi wa Maafisa Utamaduni, Sanaa na Michezo Katika ngazi za Mikoa na Halmashauri baada kuanzishwa Kitengo Kipya katika ngazi hizo katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa.		Desemba, 2023		Juni, 2024	Mikoani	DME DPP MUT MMS MMM
19.	Utekelezaji wa maelekezo		Desemba,	Machi, 2024	Juni, 2024	Dodoma	DME

Na.	Eneo Litakalofanyiwa Ufuatiliaji na Tathmini	Muda wa Utekelezaji na Tathmini				Mahali/Mkoa	Mhusika
		Robo ya I (Julai – Septemba, 2023)	**Robo ya II (Oktoba – Desemba, 2023)**	**Robo ya III Januari – Machi, 2024)**	**Robo ya IV (Aprili – Juni, 2024**		
	mahsusi ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii		2023				DPP MUT MMS MMM
20.	Utekelezaji wa Maazimio na yatokano na vikao vya Baraza la Wafanyakazi		Septemba, 2023		Aprili, 2024	Dodoma	WAKUU WA IDARA NA VITENGO; KATIBU - BLW
21.	Tathmini ya Mfuko wa Kufarijiana na SACCOS ya Wizara		Septemba, 2023		Aprili, 2024	Dodoma	DAHRM
22.	Tathmini ya utekelezaji wa ukabilianaji wa vihatarishi			Januari, 2024	Juni, 2024	Dodoma	DME DPP
23.	Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Ununuzi wa Wizara wa mwaka 2022/23		Desemba, 2023		Juni, 2024	Dodoma	DME DPMU
24.	Tathmini ya Utekelezaji wa Hoja za Ukaguzi kutoka CAG	Septemba, 2023	Desemba, 2023	Machi, 2024	Juni, 2024	Dodoma	CA DPP MMM MUT MMS DAHRM DPMU
25.	Tathmini ya usimamizi wa masuala ya fedha na manunuzi katika Wizara		Desemba, 2023		Juni, 2024	Dodoma	CIA CA DPMU

Na.	Eneo Litakalofanyiwa Ufuatiliaji na Tathmini	Muda wa Utekelezaji na Tathmini				Mahali/Mkoa	Mhusika
		Robo ya I (Julai – Septemba, 2023)	**Robo ya II (Oktoba – Desemba, 2023)**	**Robo ya III Januari – Machi, 2024)**	**Robo ya IV (Aprili – Juni, 2024**		
26.	Ufuatiliaji wa viashiria vya Mkataba wa Utendajikazi	Septemba, 2023	Desemba 2023	Machi, 2024	Juni, 2024	Dodoma	DPMU DAHRM
27.	Tathmini ya matamasha mbalimbali yanayoratibiwa na Wizara		Desemba, 2023		Mei, 2024	DSM Dodoma	DME DPP MUT MMS MMM
28.	Tathmini ya Ufanisi wa Timu za Taifa katika mashindano ya Kikanda na Kimataifa.	Septemba, 2023	Desemba, 2023	Januari, 2024	Juni, 2024	DSM Dodoma	DME MMM
29.	Kitengo cha Sheria kushirikiana na Idara za Kisekta kufuatilia na kutathmini michakato ya utungaji na urekebu wa sheria, Kanuni na miongozo mbalimbali inayoandaliwa na Idara na Taasisi zilizopo chini ya Wizara	Septemba, 2023	Desemba, 2023	Machi, 2024	Juni, 2024	**Dodoma**	DLS MUT MMS MMM
30.	Kufanya ufuatiliaji na Tathmini ya utekelezaji wa mikataba mbalimbali ya Ushirikiano baina ya Wizara na nchi/mashiriki mbalimbali.	Septemba, 2023	Desemba, 2023	Machi, 2024	Juni, 2024	**Dodoma**	DME DLS MUT MMS MMM

SEHEMU YA TATU

MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIWA KATIKA UFUATILIAJI NA TATHMINI

3.1 Utangulizi

Shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika Wizara na Taasisi zilizo chini yake zitatekelezwa kwa ufanisi na tija ikiwa watekelezaji kutoka Idara na Vitengo watazingatia masuala muhimu/utaratibu utakaofanikisha utekelezaji wa shughuli hizo. Baadhi ya masuala ya kuzingatiwa ni kama ifuatavyo: -

3.2 Majukumu ya Uratibu na Usimamizi wa Shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini

(a) **Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini** ndio mratibu mkuu na msimamizi wa shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika Wizara. Kitengo hiki kitahusika na uratibu wa uandaaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini na kuziwasilisha katika vikao vya Menejimenti ya Wizara.

(b) **Idara na Vitengo,** vitatekeleza shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika maeneo yao kulingana na majukumu wanayoyatekeleza, zitaandaa taarifa za ufuatiliaji na tathmini na kuwasilisha taarifa hizo katika Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya uratibu. Pia, zitashiriki katika shughuli mbalimbali za ufutiliaji na tathmini kwa utaratibu utaopendekezwa.

(c) **Menejimenti ya Wizara:** Menejimenti ya Wizara ina jukumu la kupitia, kujadili na kuidhinisha shughuli na taarifa za ufuatiliaji na tathmini. Aidha, Menejimenti ina jukumu la kuhakikisha hatua zinachukuliwa kulingana na mapendekezo ya taarifa za ufuatiliaji na tathmini. Hivyo, vikao vya mapitio ya ‘Menejimenti’ vya kujadili taarifa za ufuatiliaji na tathmini vitafanyika na kuhakikisha hatua stahiki zinachukuliwa kutokana na maazimio ya vikao hivyo.

3.3 Kujenga uwezo wa Watumishi wa Wizara katika masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini

Idara na Vitengo vitakuwa na jukumu la kujenga uwezo wa watumishi walio chini yao ili waweze kushiriki na kufanya ipasavyo shughuli za ufutiliaji na tathmini. Aidha, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kitahusika katika kuwezesha kutoa utaalam kwa Idara na Vitengo katika kufanya shughuli za ufuatiliaji na tathmini.

3.4 Utaratibu wa Idara/ Vitengo na Wadau Wengine Kushiriki katika Ufuatiliaji na Tathmini

Idara na Vitengo vitaunda Timu za ufuatiliaji wa tathmini kwa kushirikiana au kwa uratibu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini. Aidha, endapo kutakuwa na uhitaji wa kushirikisha Taasisi nyingine, Taasisi hizo zitashirikishwa kwa kibali cha Katibu Mkuu.

3.5 Mtiririko wa Hatua za Utekelezaji wa Shughuli za Ufuatiliaji na Tathmini

Na.	Hatua	Maelezo
1.	Kuandaa hadidu za rejea (ToRs)	Kuainisha hadidu za rejea (ToRs) kwa kuzingatia aina, hitaji au lengo la shughuli ya ufuatiliaji na tathmini.
2.	Upangaji na Uandaaji wa Bajeti	Bajeti itaandaliwa kulingana na hadidu za rejea zilizoainishwa. Bajeti husika itazingatia aina ya ufuatiliaji na tathmini inayotarajiwa kufanyika.
3.	Muundo wa Timu ya wataalam wa ufuatiliaji na tathmini	Timu ya ufuatiliaji na tathmini itazingatia shughuli inayofanyiwa ufuatiliaji na tathmini na hadidu za rejea kuunda timu ya wataalam.
4.	Kutembelea na Kukusanya taarifa	Timu itakusanya taarifa kulingana lengo la ufuatiliaji na tathmini. Hatua hii itahusisha:- *Kukagua, mahojiano, na mapitio ya nyaraka mbalimbali za Mradi*
5.	Uchambuzi na uchakataji wa taarifa	Timu itachakata na kuchambua taarifa zilizokusanywa na kuandaa taarifa ya ufuatiliaji tathmini.
6.	Uandaaji wa taarifa na maoni	Timu itaandaa taarifa itakayoonesha hatua ya utekelezaji na matokeo yaliyofikiwa, changamoto zilizopo na mapendekezo kwa kuzingatia maoni ya wadau kwa kadri itakavyoweka na. Aidha, taarifa itawasilishwa katika kikao cha Menejimenti kwa ajili ya kujadiliwa na hatua za utekelezaji.

Kiambatisho Na. 1 ni mfano wa Masuala ya Kuzingatia pamoja na Hadidu za Rejea kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini ya miradi ya maendeleo.

3.6 Zana kwa Ajili ya Ufuatiliaji na Tathmini

Zana *(tools)* za ufuatiliaji na tathmini zinazo tumika ni pamoja na:

(a) **Orodha ya Rejea "Checklist":** Taarifa muhimu kuhusu mradi au shughuli inayofanyiwa ufuatiliaji na tathmini zitaorodheshwa. Mfano wa masuala ambayo yanaweza orodheshwa ni nyaraka za miradi, taarifa za utekelezaji, mtiririko wa fedha, mpango kazi, uridhikaji na matarajio kwa wanufaika wa mradi, Hali ya usimamizi wa huduma, changamoto zilizopo na mapendekezo ya kukabiliana nazo. Kiambatisho Na. 2 ni mfano wa orodha ya rejea kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini za miradi ya maendeleo. **Kwa kuzingatia mfano wa Kiambatisho Na. 2**, Idara na Vitengo vitaandaa orodha rejea zinazokidhi mahitaji ya kazi zitakazofanyiwa ufuatiliaji na tathmini; na

(b) **Dodoso *"Questionnaire"*:** Timu itaandaa maswali yaliyopangiliwa au yasiyopangiliwa ambayo yatatumika kwenye mahojiano na majadiliano ili kuongoza upatikanaji wa taarifa kutoka kwa wadau.

3.7 Muundo wa Taarifa ya Ufuatiliaji na Tathmini

Taarifa za ufuatiliaji na tathmini itaandaliwa kwa kupitia mpangilio Utangulizi (maelezo mafupi yatakayoelezea shughuli inayofanyiwa ufuatiliaji au tathimi na madhumini yake. Aidha, kiainishwe kipindi kinachofanyiwa ufuatiliaji na tathmini); (ii)

Taarifa za Fedha za utekelezaji (ikijumuisha vyanzo vya fedha, fedha zilizotolewa, zolitumika, bakaa na sababu ya kutumika. Aidha, taarifa za fedha zitawekwa kulingana na aina ya shughuli inayofanyiwa ufuatiliaji au tathmini; (iii) Watakelezaji na wanufaikaji wa shughuli husika; (iv) Hatua iliyofikiwa kwa kuainisha asilimia ya jumla iliyofikiwa na shughuli zilizofanyika; na maeneo yaliyobainika (Aidha, yaelezwe masuala kuhusu utekelezaji na fedha zilizotolewa); Vile vile picha zinazoonesha hali ya utekelezaji, picha kutoka kwa wanufaika au eneo la utekelezaj zijumuishwe; (v) changamoto za utekelezaji na mapendekezo ya hatua za kukabiliana nazo; (vi) Masuala ambayo Timu imejifunza (mafunzo ya Ufuatiliaji na Tathmini); na (vii) Hitimisho.

3.8 Ufuatiliaji wa Viashiria

Idara na Vitengo kwa uratibu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini vitafanya ufuatiliaji wa **viasharia vya kupima utendaji kazi** kwa kuzingatia mkataba wa Utendaji kazi *(Performance Contracting)* wa mwaka 2023/24 uliowasilishwa na Idara na Vitengo.

3.9 Ufuatiliaji na tathmini ya Vihatarishi

Idara na Vitengo kwa uratibu wa Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmni pamoja na Idara ya Sera na Mipango vitakuwa na jukumu la kufanya ufuatiliaji na tathmini ya ukabilianaji wa vihatarishi ambavyo vimeainishwa katika mwongozo wa vihatarishi (*'risk framework)* na rejesta ya vihatarishi (*risk rejister')*. Masuala yatakayozingatiwa ni pamoja na kuangalia kama mikakati ya kukabiliana na viashiria inatekelezwa, changamoto zilizopo, na mapendekezo kukabiliana nazo.

3.10 Tathmini

Tathmini zitakazoandaliwa, pamoja na masuala mengine zizingatie matumizi ya rasilimali, jitihada zilizofanyika, ufikiwaji wa malengo na mafanikio yaliyopatikana, ufanisi, matokeo katika muda wa kati na mrefu ikilinganishwa na malengo yaliyopangwa, kujifunza, uendelevu na athari katika muda wa kati au mrefu. Tathmini hizi zitajumuisha kupitia taarifa mbalimbali za utekelezaji, na kufanya mahojiano na wahusika au wanufaika.

Tathmini zinaweza kufanywa na kusimamiwa na timu itakayoundwa na Wizara au kushirikisha au kufanywa na Mtaalam Elekezi kutoka nje ya Wizara ambapo Wizara itaandaa Dondoo za Rejea zitakazo ongoza tathmini.

3.11 Taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini

Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kitaratibu maandalizi ya taarifa jumuishi za kila robo mwaka za Ufuatiliaji na Tathmini na kuwasilisha katika ngazi mbalimbali Serikalini kwa kuzingatia miongozo ya utekelezaji wa shughuli za Serikali ikijumuisha: Sheria ya Bajeti Sura 439; Sheria ya Fedha za Umma, Sura 348; Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2022/23; Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini

katika Utumishi wa Umma; Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi na programu za Maendeleo; na Mkakati wa ufuatiliaji wa Tathmini za Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano - FYDP III (2021/22-2025/26).

3.12 Utaratibu wa Upatikaji wa Fedha za Utekelezaji wa Mpango wa Ufatiliaji na Tathmini kwa Mwaka 2023/24

Idara/Kitengo kitagharamia shughuli za ufuatiliaji na tathmini. Aidha, Idara, Vitengo na Taasisi vinaweza kuchangia gharama ikiwa shughuli za ufuatiliaji au tathmini zitafanyika kwa ushirikiano, hivyo gharama za ufuatiliaji na tathmini kulipwa na Idara/ Kitengo husika. Aidha, Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kwa kushirikiana na Idara ya Sera na Mipango kitaendelea kutafuta rasilimali za ziada kwa ajili ya kugharamia shughuli za ufuatiliaji na tathmini katika Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara.

SEHEMU YA NNE

HITIMISHO

Kwa kuzingatia Malengo Makuu ya Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Uongozi Mahili wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano, 2021/2022 – 2025/26, Mpango Kazi wa ufuatiliaji na Tathmini utakuwa zana muhimu kufanikisha malengo ya Wizara. Hivyo, wadau wote muhimu katika utekelezaji wa mpangokazi wanahimizwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Mpango Kazi wa kutekeleza shughuli husika kwa mujibu wa ratiba iliyopangwa.

MASUALA MUHIMU YA KUZINGATIA WAKATI WA KUFUATILIA NA KUTATHMINI UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

A. UTANGULIZI

Kitengo cha Ufuatiliaji na Tathmini kina jukumu la kuratibu ufuatiliaji na tathmini ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo. Katika kutekeleza jukumu hilo, Kitengo kinafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo kila robo mwaka. Miradi inayofuatiliwa ni ile inayogharamiwa kwa fedha za ruzuku ya Serikali Kuu na ile inayotekelezwa na fedha za Taasisi zilizo chini ya Wizara. Kwa msingi huo, Kitengo kinafanya ufuatiliaji kila robo ya mwaka 2023/24.

B. LENGO LA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MIRADI

(a) Kupata uelewa wa eneo la mradi na kubaini hatua zilizofikiwa katika utekelezaji;
(b) Kuelewa changamoto za utekelezaji wa miradi na kupendekeza hatua stahiki za namna ya kukabiliana nazo;
(c) Kubaini mchango wa mradi katika kutekeleza Mpango na Bajeti ya Wizara;
(d) Kupata taarifa za msingi kwa ajili ya maandalizi ya Mpango na Bajeti katika mwaka wa fedha unaofuata;
(e) Kupata taarifa ambazo zitasaidia katika uombaji wa rasilimali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutoka Hazina;
(f) Kuongeza uwajibikaji katika matumizi ya rasilimali za Umma;
(g) Kuweka mkazo kwenye kufikia malengo tarajiwa; na
(h) Kusaidia kwenye utoaji wa maamuzi sahihi.

C. HADIDU ZA REJEA KWA AJILI YA UFUATILIAJI NA TATHMINI YA MIRADI

(a) Kuainisha kiasi cha fedha zilizotengwa na zilizopokelewa;
(b) Kufuatilia fedha zilizopokelewa iwapo zimetumika katika utekelezaji wa mradi kama ilivyokusudiwa;
(c) Kukagua na kubainisha kazi zilizotekelezwa na gharama zake kwa mujibu wa mikataba;
(d) Kupitia na kutathmini maeneo yote ya utekelezaji (ujenzi) wa mradi kwa mujibu wa michoro;
(e) Kufuatilia iwapo utekelezaji mradi umezingatia Mpango Kazi wa utekelezaji;
(f) Kutathmini usimamizi wa mradi ulivyofanyika na ubora wa kazi zilizotekelezwa;
(g) Kubaini changamoto za utekelezaji wa miradi na kupendekeza namna bora ya kuzitatua;

(h) Kuainisha mchango wa mradi katika utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka husika; na

(i) Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya ufuatiliaji wa miradi kwa Katibu Mkuu na katika kikao cha Menejimenti kadri itakavyoelekezwa..

D. **NJIA ZITAKAZOTUMIKA**

(a) Kupitia na kuchambua nyaraka na taarifa mbalimbali (Mpango na Bajeti ya mwaka husika, Taarifa za Utekelezaji za robo mwaka, Taarifa za Mshauri Elekezi, Taarifa za Vikao vya Kamati za Mradi, Mikataba ya Wakandarasi na Washauri Elekezi, Mpango kazi na Mpango wa Mtiririko wa Fedha wa mwaka husika);

(b) Taarifa ya utolewaji wa fedha kutoka Hazina kwa kila mradi;

(c) Kitabu cha kumbukumbu za zabuni ya miradi *(Procurement Register)*;

(d) Kufanya majadiliano na wadau muhimu; na

(e) Kutembelea maeneo ya utekelezaji kwa lengo la kujiridhisha na kujionea hali halisi.